UWAJIBIKAJI

# Bei dawa za mifugo yamshtua Ulega

**Halmashauri imeagizwa kutumia idara ya mifugo kununua dawa hizo**

Rajabu Athumani, Mwananchi
rathumani@mwananchi.co.tz

**Handeni.** Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega ameutaka uongozi wa halmashauri ya mji Handeni mkoani Tanga, kuangalia upya bei ya dawa za mifugo kwani kuna wafanyabiashara wanaowalangua wafugaji.

Akihutubia wananchi wilaya ya Handeni jana katika soko la mifugo la Ndelema, Ulega alisema amepata taarifa kuna wafanyabiashara wameongeza bei dawa za mifugo tofauti na bei elekezi.

Ulega alisema tabia hiyo haitavumiliwa hivyo uongozi wa halmashauri uangalie utaratibu wa kununua dawa kupitia idara ya mifugo, kisha kuwauzia wafugaji kwa bei watakayomudu.

Alisema dawa zinazotengenezwa nchini hakuna sababu ya kupandishwa bei, kwani hakuna gharama za ziada.

"Taarifa niliyonayo ni Handeni yapo maduka ya dawa za mifugo na kilimo yanapandisha bei, zipo dawa zinatakiwa kuuzwa kwa Sh1,500 lakini zinauzwa kwa Sh8,000 hii haikubaliki lazima hatua zichukuliwe," alisema Ulega.

Awali, katibu tawala wilaya ya Handeni, Bonifare Maiga alikiri mnada wa Nderema kukabiliwa na changamoto hiyo ingawa za juu zinapaswa namna ya kusaidia nilipo tegemeo la halmashauri.

Maiga alisema uongozi wa wilaya katika kuboresha mnada huo umefuta ushuru kwa wafanyabiashara ambao wanaingiza mifugo mnadani, kwani imebainika wapo ambao hawauzi kwa utaratibu wa awali walikuwa wakilipishwa.

Alisema kati ya ng'ombe 850 wanaopelekwa mnadani hapo wanaweza kuuzwa 650, mbuzi 550 wanauzika wote na kondoo kati 250 wanaweza kuuzwa 150.

Naye mwenyekiti wa wafugaji mnada wa Nderema, Abdi Madeni alisema zipo kero nyingi na kuomba uongozi wa halmashauri kuzitatua haraka.

Alisema mnada huo hauna uzio hivyo usalama wa wafanyabiashara ni mdogo, mifugo inapitishwa njia zisizo rasmi huku barabara za kuingia zikiwa mbovu.

Mfugaji kutoka Msomera Samboni Sinyambu alisema alinunua dawa ya mapafu kwa Sh12,000 ilihali bei halali ni Sh6,000.

> "Taarifa niliyonayo ni Handeni yapo maduka ya dawa za mifugo na kilimo yanapandisha bei, zipo dawa zinatakiwa kuuzwa kwa Sh1,500 lakini zinauzwa kwa Sh8,000 hii haikubaliki lazima hatua zichukuliwe."
>
> **Ulega**



Naibu waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega akifurahia jambo na wananchi wa Kwamatuku wilayani Handeni mkoani Tanga jana. **Picha na Rajabu Athumani**

nayedaiwa kuu...

Scanned by CamScanner